TANGAZO LA SERIKALI NA. 513 la tarehe 21/05/2024

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16(1))*

SHERIA NDOGO YA USHURU WA HUDUMA YA HALMASHAURI YA JIJI LA ARUSHA YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ushuru wa Huduma ya Halmashauri ya Jiji la Arusha ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Jiji la Arusha.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"biashara" maana yake ni uendeshaji wa shughuli yoyote halali inayomwingizia mtu, kikundi, kampuni au taasisi kipato;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Jiji ya Arusha;

"hesabu" maana yake ni jumla ya mauzo katika kipindi cha siku, mwezi au miezi mitatu katika mwaka husika wa mapato;

"hesabu za mwisho" maana yake ni hesabu

zinazowasilishwa na taasisi yoyote ya kibiashara baada ya kipindi cha hesabu pamoja na nyaraka au maelezo yatakayotakiwa kutolewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

Sura ya 212

"kampuni" maana yake ni kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Kampuni;

"kipindi maalumu cha hesabu" maana yake ni muda ambao mfanyabiashara anatakiwa kuwasilisha hesabu za biashara kwa Halmashauri;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Jiji ya Arusha au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi chini ya Sheria Ndogo hii;

"mlipa ushuru wa huduma" maana yake ni kampuni, tawi la kampuni au mfanyabiashara mwenye leseni anayefanya shughuli zake katika eneo la Halmashauri;

"tawi la kampuni" maana yake ni tawi la kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Kampuni;

"ushuru wa huduma" maana yake ni ushuru unaotozwa na kukusanywa na Halmashauri kutoka kwa kampuni, tawi la kampuni au mfanyabiashara yeyote mwenye leseni ya biashara ambaye mauzo yake kwa mwaka ni zaidi ya shilingi milioni nne;

Sura ya 212

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi au kikundi cha watu, kampuni au shirika ambalo limeteuliwa na Halmashauri kufanya kazi yoyote chini ya Sheria Ndogo hii kwa niaba ya Halmashauri.

Ushuru wa huduma

4.-(1) Halmashauri itatoza na kukusanya ushuru wa huduma kwa kiwango cha asilimia sifuri nukta tatu ya mauzo baada ya kutoa kodi ya ongezeko la thamani na ushuru wa bidhaa kutoka kwa mtu yeyote mwenye leseni ya biashara anayewasilisha hesabu za mauzo kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1),

Halmashauri itatoza na kukusanya ushuru wa huduma kwa kiwango kilichoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii kutoka kwa wafanyabiashara wenye leseni za biashara ambao hawawasilishi hesabu za mauzo Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Wajibu wa mlipa ushuru wa hudum

5.-(1) Kila mlipa ushuru wa huduma atakuwa na wajibu wa-

(a) kulipa ushuru wa huduma kwa kiwango kilichoainishwa katika Sheria Ndogo hii;
(b) kuwasilisha taarifa sahihi za mauzo ya kila mwezi endapo anawasilisha taarifa za hesabu za mauzo kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania;
(c) kuwasilisha hesabu sahihi na za kweli;
(d) kuwasilisha nyaraka au taarifa inayotakiwa kuwasilishwa kwa Halmashauri katika muda ulioainishwa;
(e) kutunza kumbukumbu za kitabu cha hesabu; na
(f) kuonesha kumbukumbu yoyote au nyaraka kwa ajili ya ukaguzi.

(2) Mlipa ushuru wa huduma atapaswa kulipa ushuru wa huduma ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya kuwasilisha taarifa za mauzo ya kila mwezi.

(3) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (2), Halmashauri inaweza kukubaliana na mlipa ushuru wa huduma juu ya utaratibu wa kulipa ushuru

(4) Mlipa ushuru atapaswa kuwasilisha Halmashauri hesabu za awali na kulipa ushuru wa huduma katika kila kipindi cha miezi mitatu katika mwaka wa fedha wa Serikali.

(5) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (4), mlipa ushuru atapaswa kuwasilisha Halmashauri hesabu za mwisho ndani ya miezi mitatu tangu kumalizika kwa mwaka wa fedha wa Serikali.

(6) Endapo mlipa ushuru hajawasilisha hesabu za mwisho kwa mwaka wa fedha husika na ametakiwa

kufanya hivyo kwa notisi ya siku thelathini, Mkurugenzi anaweza, kwa kadri atakavyoona inafaa, kuamua kiwango cha hesabu za mlipa ushuru husika kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(7) Ushuru uliothaminiwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, utalipwa ndani ya siku thelathini tangu tarehe ya tathmini.

(8) Endapo mlipa ushuru hajawasilisha majumuisho ya hesabu zake kwa mwaka wa mapato, na endapo Mkurugenzi au Afisa Mwidhiniwa ana maoni kuwa mlipa ushuru husika ana wajibu wa kulipa ushuru kwa mwaka huo, anaweza kwa kadri atakavyoona, kuamua kiwango cha hesabu za mlipa ushuru huyo:

Mamlaka ya Mkurugenzi

6.-(1) Endapo mlipa ushuru wa huduma anayepaswa kuwasilisha taarifa ya mauzo chini ya Sheria Ndogo hii atashindwa kuwasilisha taarifa sahihi za mauzo kwa wakati, Mkurugenzi anaweza kutoa notisi ya kumtaka mlipa ushuru wa huduma kuwasilisha taarifa hiyo ndani ya siku thelathini kuanzia tarehe ya kutolewa kwa notisi.

(2) Mkurugenzi anaweza kumtaka kwa maandishi mtu yeyote mwenye taarifa kuhusu mfanyabiashara anayepaswa kulipa ushuru wa huduma kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kuwasilisha kwake taarifa ambazo zitatumika kama taarifa sahihi.

(3) Mkurugenzi anaweza kumwagiza kwa maandishi Afisa Mwidhiniwa kuingia kwenye jengo au eneo la mlipa ushuru wa huduma kwa nia ya kufanya uchunguzi na tathmini ya kumbukumbu za biashara, vitabu vya hesabu na taarifa kwa ajili ya kupata au kujua kiwango sahihi cha ushuru anachopaswa kulipa.

(4) Mkurugenzi anaweza kumteua kamishna wa kodi ya forodha au kodi ya mapato kwa ajili ya kutathmini na kukusanya ushuru wa huduma na kuwasilisha kwa Halmashauri kwa lengo la kupata ushuru wa huduma pamoja na madeni yake.

(6) Mkurugenzi, kwa taarifa ya maandishi, anaweza kumtaka mlipa ushuru yeyote kuwasilisha hesabu zenye taarifa kamili za shughuli za kibiashara zikionesha thamani ya kiasi na thamani ya kifedha ya bidhaa au huduma zilizozalishwa, kutolewa, kusambazwa au kuuzwa kibiashara na taarifa ya fedha katika kipindi maalumu kisichozidi siku thelathini tangu tarehe ya taarifa hiyo.

(8) Mkurugenzi anaweza kwa taarifa ya maandishi ya siku saba, kumtaka mlipa ushuru kuwasilisha kumbukumbu za kibiashara na vitabu vya hesabu kwa nia ya kupata taarifa kwa ajili ya kufanyiwa tathmini au kukusanya ushuru wa huduma.

Uteuzi wa Wakala

7.-(1) Halmashauri inaweza kuteua Wakala wa kukusanya ushuru kwa niaba yake.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) atakuwa na wajibu wa-

(a) kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoidhinishwa katika Sheria Ndogo hii; na
(b) kukusanya ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Mamlaka ya Afisa Mwidhiniwa

8. Afisa Mwidhiniwa anaweza-

(a) kupokea na kukubali hesabu za mlipa ushuru na kuzifanyia tathmini kuhusu kiwango cha hesabu cha mlipa ushuru endapo hesabu hizo zitakuwa si sahihi; au
(b) kukataa hesabu za mwisho iwapo atakuwa na sababu za msingi za kuamini kuwa hesabu hizo si sahihi.

Ukokotoaji wa ushuru wa

9. Halmashauri itakokotoa ushuru wa huduma wa

huduma

mlipa ushuru anayewasilisha taarifa za mauzo Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kuzingatia taarifa zinazowasilishwa na mlipa ushuru wa huduma katika kipindi maalumu cha hesabu.

Makosa

10. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo-

(a) atashindwa kuwasilisha Halmashauri taarifa sahihi za mauzo katika muda ulioainishwa katika Sheria Ndogo hii;
(b) atawasilisha Halmashauri taarifa zisizo sahihi;
(c) atashindwa kulipa ushuru wa huduma katika muda ulioainishwa katika Sheria Ndogo hii;
(d) atamshawishi mlipa ushuru wa huduma kukataa au kukwepa kulipa ushuru;
(e) atamzuia Afisa Mwidhiniwa au Wakala wa Halmashauri kutekeleza masharti ya Sheria Ndogo hii; au
(f) atatoa taarifa isiyo sahihi kuhusu ulipaji wa ushuru.

Adhabu

11. Mtu atakayepatikana na hatia kwa tenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au adhabu zote mbili.

Kufifilisha kosa

12. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kinyume na Sheria Ndogo hii kiasi kisichozidi shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalumu iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii na kulipa ushuru anaodaiwa.

Kufutwa kwa Sheria Ndogo T.S Na. 11 la 2004

13. Sheria Ndogo za (Ushuru wa Huduma) za Halmashauri ya Manispaa ya Arusha za Mwaka 2004 zinafutwa.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4(2))*

USHURU WA HUDUMA KWA WAFANYABIASHARA WENYE LESENI ZA BIASHARA AMBAO HAWAWASILISHI HESABU ZA MAUZO MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

| Na. | Aina ya Biashara | Kiwango cha Ushuru kwa Mwaka (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Baa kubwa | 600,000/= |
| 2. | Baa ya kati | 240,000/= |
| 3. | Baa ndogo | 120,000/= |
| 4. | Eneo la kuoshea magari | 120,000/= |
| 5. | Duka la rejareja mjini | 120,000/= |
| 6. | Duka la rejareja nje ya mji | 60,000/= |
| 7. | Hardware ndogo | 120,000/= |
| 8. | Wakala wa Fedha mtandao na LUKU | 100,000/= |
| 9. | Duka la spea za magari au pikipiki | 240,000/= |
| 10. | Salon kubwa | 120,000/= |
| 11. | Salon ndogo | 60,000/= |
| 12. | Duka la jumla la mitumba | 600,000/= |
| 13. | Duka kubwa la nguo | 600,000/= |
| 14. | Karakana ya kuranda mbao katikati ya mji | 240,000/= |
| 15. | Karakana ya kuranda mbao nje ya mji | 120,000/= |
| 16. | Karakana au duka la samani (kijiwe) | 180,000/= |
| 17. | Karakana au duka la samani (kubwa) | 600,000/= |
| 18. | Karakana ya shughuli za kuchomelea (welding au aluminium) | 300,000/= |
| 19. | Kampuni au ofisi ya wanasheria au wakili | 150,000/= |
| 20. | Biashara ya magodoro | 140,000/= |
| 21. | Biashara ya matofali | 300,000/= |
| 22. | Duka dogo | 15,000/= |
| 23. | Biashara ya kukaanga viazi (chipsi) | 20,000/= |
| 24. | Duka la vifaa vya simu | 20,000/= |
| 25. | Duka la simu | 20,000/= |
| 26. | Duka la vipodozi | 20,000/= |
| 27. | Mgahawa | 20,000/= |
| 28. | Bucha | 20,000/= |
| 29. | Maua | 20,000/= |
| 30. | Duka la samaki | 20,000/= |
| 31. | Kioski | 20,000/= |
| 32. | Kiwanda cha kushona (kibanda) | 20,000/= |
| 33. | Duka la vifaa vya umeme | 20,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 34. | Sonara mdogo | 20,000/= |
| 35. | Duka la vifaa vya urembo | 20,000/= |
| 36. | Nafaka za jumla | 20,000/= |
| 37. | Gereji ya magari | 20,000/= |
| 38. | Wakusanya vyuma chakavu | 20,000/= |
| 39. | Ofisi ya Wakala wa tiketi za magari na ndege | 20,000/= |
| 40. | Mashine za kusaga na kukoboa nafaka | 20,000/= |
| 41. | Mchanga | 20,000/= |
| 42. | Kiwanda cha maandazi | 20,000/= |
| 43. | Studio | 20,000/= |
| 44. | Ofisi ya fundi umeme au bomba au vifaa vya majumbani | 20,000/= |
| 45. | Duka la kuuza mali zilizotumika | 20,000/= |
| 46. | Ofisi au kumbi ya mazoezi | 20,000/= |
| 47. | Mpambaji au mpishi | 20,000/= |
| 48. | Duka la spea za baiskeli | 20,000/= |
| 49. | Kituo cha kulea watoto (day care) | 20,000/= |
| 50. | Kumbi au bustani ya sherehe | 20,000/= |
| 51. | Duka la tiba za asili | 20,000/= |
| 52. | Kibanda cha mkaa | 20,000/= |
| 53. | Duka la gesi ya kupikia | 20,000/= |
| 54. | Duka la vifaa vya asili (vinyago, urembo na vingine) | 20,000/= |
| 55. | Duka la samani | 20,000/= |
| 56. | Kibanda cha kupiga na kusafisha picha | 20,000/= |
| 57. | Duka la shajala (Stationery) | 20,000/= |
| 58. | Kiwanda kidogo cha viatu | 20,000/= |
| 59. | Duka la tairi za gari | 20,000/= |
| 60. | Duka la tairi za pikipiki | 20,000/= |
| 61. | Duka la tairi za baiskeli | 20,000/= |
| 62. | Duka la tairi zilizotumika | 20,000/= |
| 63. | Duka la mbogamboga | 20,000/= |

---

JEDWALI LA PILI

---

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 12)*

FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ……………………………………………………… nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya …………………………………………. ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi …......…. Mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya …… ya Sheria Ndogo ya Ushuru wa Huduma ya Halmashauri ya Jiji la Arusha ya Mwaka, 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, niko tayari kulipa kiasi cha ada au ushuru ninaodaiwa pamoja na faini badala ya kushtakiwa Mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU
Leo tarehe………….ya Mwezi…………..… Mwaka …………….

Jina……………………………….. Saini………………………

MBELE YANGU:
Jina: ……………………………………..……………
Saini………………………..…………………………..
Wadhifa: …………………………………………………
Tarehe…………………………………………………….

Lakiri ya Halmashauri ya  ya Jiji la Arusha imegongwa kwenye sheria ndogo hii kufuatia Azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri Jiji la Arusha uliofanyika tarehe 03 Mwezi Novemba, 2023 na imegogwa mbele ya ;

INJ. JUMA HAMSINI
Mkurugenzi wa Jiji la Arusha

MAXIMILIAN J. IRANQHE
*Meya wa Jiji la Arusha*

NAKUBALI,

L.S

Dodoma
20 Februari, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA
*Waziri wa Nchi ofisi ya Rais*
*(Tawala za mikoa na serikali za mitaa)*